# Ulega: Saidieni wafugaji wa ng'ombe wa asili

**Sekta ya mifugo ina nafasi kubwa katika kukuza uchumi wa nchi na kuboresha ustawi wa maisha ya Watanzania, ikiwamo kuwaondoa kutoka kwenye umasikini.**

> Tuna wazalishaji wadogo wenye changamoto nyingi kama vile lishe duni, maji, afya. Tafiti, nguvu na maarifa vielekezwe katika wafugaji wa asili..."
>
> **Abdallah Ulega**

Mwandishi Wetu, Mwananchi

**Dar es Salaam.** Wakati takwimu zikionyesha wafugaji wa asili wakizalisha maziwa kati ya lita moja na nusu hadi tatu kwa siku, Naibu wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewataka watafiti katika sekta ya mifugo, kufanya tafiti zitakazokuza uzalishaji mkubwa wa maziwa nchini hasa kwa wafugaji wa asili.

Akizungumza katika mkutano wa watafiti na wadau wa maziwa uliofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam, alisema kukuza sekta ya mifugo na uvuvi, ni miongoni mwa vipaumbele vinavyoweza kuchochea ukuaji wa uchumi na kuondosha umasikini nchini.

" Tuna wazalishaji wadogo wenye changamoto nyingi kama vile lishe duni, maji, afya. Tafiti, nguvu na maarifa vielekezwe katika wafugaji wa asili ambao ndio wengi na changamoto zao," alisema.

Aliwataka wataalamu kupeleka maarifa kuhusu ufugaji bora na wenye tija wa ng'ombe hadi kwa wafugaji wa chini ambao baadhi ni wazito katika kukubali mabadiliko ikiwamo kutumia malisho ya kupanda.

" Fursa ya nyama na maziwa ni kubwa. Wimbo wetu uwe ni ufugaji kibiashara tutoke katika makundi makubwa ya ng'ombe, tuelekee katika ufugaji wa kibiashara," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu, wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania, Profesa Erick Komba, alisema watafiti wamefanya utafiti kuhusu namna ya kupunguza hewa ukaa inayozalishwa na mifugo na hivyo kuongeza athari katika mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema kama wafugaji nchini watajihimu kutumia mbari bora na malisho yaliyoboreshwa, wana uwezo wa kuongeza uzalishaji mara mbili na pia kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Scanned with CamScanner

# Sekta ya mifugo yakabiliwa kero magonjwa

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

SEKTA ya mifugo nchini bado inakabiliwa na kero nyingi ikiwamo magonjwa kwa mifugo.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Amos Zephania, aliyasema hayo katika kongamano la saba la wadau wa kilimo, jijini hapa.

Alisema, kutokana na hali hiyo wizara inatoa wito kwa wadau mbalimbali kuwekeza katika kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa dawa za mifugo ili kukabili kero hiyo.

Alisema kero nyingine ni upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo hali ambayo imekuwa sababu kubwa inayoathiri sana sekta hiyo nchini.

"Wakati wa masika hata ng'ombe wale wa kienyeji utoaji wa maziwa unaongezeka, lakini wakati wa kiangazi kiwango cha maziwa kinashuka hii ni kutokana na uhaba wa maji pamoja na malisho ya mifugo yetu hivyo nitoe wito kwa wadau kutafuta namna ya kuzalisha malisho," alisema Zephania.

Alisema pia ipo haja ya kuboresha mifugo inayozalishwa nchini ili kuendana na mahitaji ya sasa.

"Ng'ombe tuliona hivi sasa nchini ni wadogo sana hawatoi maziwa ya kutosha, lakini hata nyama yao ni kidogo sana ambayo haiwezi kuleta ushindani katika soko hivyo ipo haja kutafuta namna ya kuboresha mifugo hii," alisisitiza.

Kadhalika, alisema kero nyingine ni uhaba wa maofisa ugani nchini kwa kuwa wanaohitajika ni 17,000 na waliopo ni 3,397 ambao hawakidhi mahitaji.

Alisema kutokana na tatizo la uhaba wa wagani wizara imeamua kuanzisha mfumo wa M-Kilimo ambao utawawezesha wakulima kupata taarifa mbalimbali zitakazo wasaidia kupata majibu ya maswali yao.

Vile vile, alisema ili kuboresha mazingira na kuwezesha ukuaji wa sekta ya mifugo katika mwaka wa fedha 2020/21 wizara imeendelea kupitia sheria za sekta ya mifugo na kanuni mpya nne zimeandaliwa na kutangazwa kwenye gazeti la serikali.

Scanned with CamScanner

Ndone. (Picha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi).

# Ng'ombe kuvalishwa hereni

**Na Peti Siyame, Nkasi**

SERIKALI imesema itafanya kampeni ya kutambua, kusajili na kufuatilia mifugo kielektroniki katika mikoa yote.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema uzinduzi wa kampeni hiyo utafanyika wilayani Nkasi na kwamba awali, itafanyika katika mikoa ya Rukwa, Katavi Kigoma na Tabora na hadi Agosti mwakani, ng'ombe wote nchini watakuwa wamevikwa hereni.

Alibainisha hayo alipozungumza na wafugaji katika kikao kilichofanyika katika Mji Mdogo wa Namanyere.

Alisema kampeni hiyo itafanywa kwa kuzingatia Sheria Namba 12 ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji ya Mwaka 2010.

Alizitaja faida za kuvisha ng'ombe hereni kuwa ni kuongeza thamani ya mifugo katika masoko ya ndani na nje ya nchi, kudhibiti wizi wa mifugo na pia idadi ya ng'ombe nchini kufahamika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma za Mifugo Tanzania, Profesa Hezron Nonga alisema katika kipindi cha 2015/16 na 2016/17 ng'ombe 17,000,000 walipigwa chapa ya moto nchi nzima na robo tatu ya hao alama zilifutika.

"Kuwapiga chapa ya moto wanyama kulisababisha asilimia 90 ya ngozi kukosa masoko ya uhakika na ushindani kwa kukosa ubora," alisema Profesa Nonga.

Scanned with CamScanner